



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI



Tarehe 28, Agosti. 2023

TANGAZO LA MNADA WA MALI CHAKAVU

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inawatangazia wananchi wote kuwa tarehe 15, Septemba. 2023 inatarajia kuuza mali chakavu kwa mnada wa hadhara utakaofanyika katika eneo la BRELA lililopo ADA Estate Kinondoni, Kiwanja (*Plot*) Na. 45 Kinondoni Shamba, Dar Es Salaam. Mali chakavu zitakazouzwa ni vifaa vya TEHAMA (ICT), Kangavuke (Generator), Samani mbalimbali na vifaa vya Ofisi.

BRELA inawaalika wananchi wote wenye nia ya kushiriki katika mnada huo tarehe 11, Septemba. 2023 na tarehe 12, Septemba. 2023 katika eneo BRELA lililopo ADA Estate Kinondoni/Shamba na Jengo la Ushirika zilipokuwa Ofisi za zamani za BRELA, kufika kufanya ukaguzi wa mali hizo.

Tarehe 11, Septemba. 2023 itakuwa siku ya ukaguzi wa kangavuke (Generator) ambao utafanyika katika Jengo la Ushirika zilipokuwa Ofisi za zamani za BRELA. Tarehe 12, Septemba. 2023 itakuwa siku ya kufanya ukaguzi wa vifaa vya TEHAMA, samani za ofisini na vifaa mbalimbali vya ofisi. Ukaguzi huu utafanyika katika eneo la ADA Estate plot namba 45, Kinondoni Shamba kilipo kiwanja cha BRELA.

Mali chakavu zitakazouzwa kwa njia ya mnada wa hadhara ni kama zilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo:-

Kundi la Mali	Idadi	Mahali Mali ilipo	Tarehe ya Mnada	Muda wa Mnada
Kangavuke	01	Jengo la Ushirika, Mnazi Mmoja-Mtaa wa Lumumba	15/09/2023	8:00 mchana
Samani	92	ADA Estate Kinondoni/Shamba	15/09/2023	4:00 asubuhi

Vifaa vya TEHAMA	315	ADA Estate Kinondoni/ Shamba	15/09/2023	4:00 asubuhi
Vifaa mbalimbali vya Ofisi	114	ADA Estate Kinondoni/ Shamba	15/09/2023	4:00 asubuhi

MASHARTI YA MNADA.

1. Wananchi wataruhusiwa kuja kukagua mali hizo chakavu siku mbili (2) kabla ya mnada.
2. Kila mnunuzi wa mali chakavu atatakiwa kulipia mali aliyonunua mara tu baada ya kutangazwa kuwa mshindi.
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa au kuchukua mali chakavu mara tu baada ya kukumilisha malipo.
4. Mali chakavu ambayo haitalipiwa kwa muda huo uliopangwa itanadiwa upya.
5. Malipo yatafanyika kwa asilimia mia moja(100%) baada ya kuuza.
6. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia mia moja (100%) ya malipo kabla ya kuchukua mali chakavu.
7. Mnada utaanza saa nne (04:00) Asubuhi katika eneo la ADA Estate Kinondoni/Shamba (Plot) Kiwanja Na. 45 kilipo Kiwanja cha BRELA kwa kuuza vifaa vya TEHAMA, Samani na vifaa mbalimbali vya Ofisi. Baada ya hapo, mnada utahamia Jengo la Ushirika zilipokuwa Ofisi za zamani za BRELA saa nane (08:00) mchana kwa ajili ya kuuza Generator (kangavuke).

IMETOLEWA NA:

AFISA MTENDAJI MKUU

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA)